JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

MWONGOZO WA MATUMIZI YA TEHAMA

KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA BARA

TOLEO LA PILI

JUNI, 2026

USALAMA WA TAARIFA • UWAZI • UFANISI • MIFUMO YA KIDIJITALI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

MWONGOZO WA MATUMIZI YA TEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA BARA

JUNI, 2026

YALIYOMO

DIBAJI ii
TAFASIRI YA MANENO iv
1. UTANGULIZI 1
1.1 Chimbuko la Mwongozo 1
1.2 Malengo ya Mwongozo 2
1.3 Walengwa wa Mwongozo 3
2 HALI HALISI YA MATUMIZI YA TEHAMA 4
3 MATUMIZI YATEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA 5
3.1. Mambo ya kuzingatia kabla ya kutumia Mifumo na nyenzo za TEHAMA. 5
3.1.1. Vitendea kazi 5
3.1.2. Ununuzi wa Vitendea Kazi 8
3.1.3. Mabadiriko ya Teknolojia ya Vifaa na Nyenzo za TEHAMA 8
3.1.4. Mafunzo 8
3.1.5. Anwani ya Barua Pepe 8
3.2. Kuwasilisha taarifa kupitia Mfumo Mama wa Tume wa MUVU. 8
3.3. Msaada wa Kiufundi 8
4 MIFUMO YA TEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA 9
4.1. Mfumo wa Uendeshaji wa shughuli za Chama 9
4.2. Usalama wa Programu na Vifaa vya TEHAMA 12
5 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO 13
5.1. Wajibu wa Chama 13
5.2. Wajibu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika 13
5.3. Wajibu wa Mkaguzi wa Nje 14
5.4. Wajibu wa Watoa Huduma 14
5.5. Wajibu wa Mfilisi 14
5.6. Wajibu wa Wadau wa Maendeleo ya Ushirika 14
5.7. Muda wa kuanza kutumika 14
5.8. Mapitio 14
6 VIAMBATISHO 15
6.1. Kiambatisho Na.1: Mapendekezo ya Sifa za Kompyuta Mpakato 15
Kiambatisho Na.2: Mapendekezo ya Sifa za Kompyuta ya Mezani 15
6.2. Kiambatisho Na.3: Mapendekezo ya Sifa za Printa 17
6.3. Kiambatisho Na.4: Mapendekezo ya Sifa za POS TPS 390 17
6.4. Kiambatisho Na. 5: Mapendekezo ya Sifa za Mizani ya Kidigitali 18
6.5. Kiambatisho Na.6: Mapendekezo ya sifa za vishikwambi 20
6.6. Kiambatisho Na.7: Mapendekezo ya sifa za Simu janja za Mkononi 21


DIBAJI

Vyama vya Ushirika katika Nchi zinazoendelea na zilizoendelea vimekuwa vyombo madhubuti vinavyowaunganisha Wananchi pamoja kwa hiari, ili kufikia malengo waliyojiwekea kwa njia ya demokrasia na usawa. Kwa kutambua umuhimu wa Vyama vya Ushirika, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya uanzishwaji na uendelezaji wa Vyama vya Ushirika ili kuhakikisha Vyama vinakidhi matakwa ya Wanachama na kuchangia maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto mbalimbali katWA ika uendeshaji na usimamizi wa Vyama, kama vile Mifumo duni ya mawasiliano na uhifadhi wa nyaraka, taarifa na kumbukumbu za Vyama, baadhi ya Vyama kupata hati chafu za ukaguzi kutokana na ukosefu wa uwazi na uwajibikaji katika kutunza kumbukumbu za fedha. Changamoto hizi kwa kiasi kikubwa zinatokana na matumizi madogo ya TEHAMA katika usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika.

Katika kutatua changamoto za usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, Tume kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo imeendelea kuhamasisha matumizi ya Mifumo na Nyenzo za TEHAMA katika utoaji wa huduma. Aidha, Tume imetengeneza Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU). Mfumo huu unawezesha kufanya usajili wa Vyama kwa njia ya mtandao, kuhifadhi kumbukumbu na taarifa za Wanachama, fedha, masoko, uwekezaji, uzalishaji, sheria, mashauri, ukaguzi na taarifa nyingine muhimu kulingana na shughuli za Chama husika na Wadau. Vilevile, Mfumo unawezesha Vyama na Wanachama kupata mrejesho juu ya taarifa mbalimbali zikiwemo za usajili, masoko, malipo, uwekezaji, ukaguzi kwa njia ya mtandao na jumbe fupi kupitia simu. Aidha, Vyama vya Ushirika 3,958 sawa na asilimia 56.05 tayari vimeanza kutumia Mifumo ya TEHAMA na nyenzo za TEHAMA.

Mwongozo huu unahimiza Viongozi, Watendaji wa Vyama vya Ushirika pamoja na Wadau wa maendeleo ya Ushirika, Wizara za Kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi mbalimbali za Umma zinazofanya kazi na Vyama vya Ushirika kufuata maelekezo na utaratibu uliowekwa katika matumizi ya Mifumo ya usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na vifaa vya TEHAMA.

Iwapo teknolojia hii itatumika kwa usahihi itasaidia Vyama vya Ushirika na Serikali kwa ujumla kupunguza gharama za uendeshaji na usimamizi na kuongeza ufanisi na uwazi na Uwajibikaji sambamba na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa Wananchi na Wadau wengine, kuwezesha kujua mchango wa Ushirika katika uchumi wa Nchi. Hivyo, ni matumaini yangu kuwa, Mwogozo huu utatumiwa kikamilifu na Vyama vya Ushirika ili kuleta matokeo chanya yaliyokusudiwa.



Dkt. Benson O. Ndiege
MRAJIS WA VYAMA VYA SHIRIKA

TAFASIRI YA MANENO

Katika Mwongozo huu, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:

“Sheria” maana yake Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 Sura ya 211 [Toleo Rekebu 2023].

“Chama” maana yake ni Chama cha Ushirika kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria

“Kanuni” maana yake ni Kanuni ya Vyama vya Ushirika ya 2015.

“TEHAMA” maana yake ni Tektonologia ya Habari na Mawasiliano.

“Mfilisi” maana yake ni mfilisi wa Chama cha Ushirika aliyeteuliwa kwa mujibu ya Sheria ya Vyama vya Ushirika.

“Mifumo” maana yake ni Mifumo ya TEHAMA na programu au nyenzo za TEHAMA itakayokuwa inatumika katika Vyama vya Ushirika

“Mtendaji” maana yake ni Mwajiriwa wa Chama cha Ushirika.

“Mtoa Huduma” maana yake ni taasisi au mtu binafsi aliyeidhinishwa kutoa huduma ya TEHAMA kwenye Chama.

“Nywila” maana yake ni neno la siri linalomuwezesha mtumiaji kuingia na kutumia Mfumo.

“Uthibitisho wa aina Mbili” ni Mfumo wa usalama unaohitaji uthibitisho wa aina mbili tofauti ili kufungua akaunti yako kwa ajili ya kupunguza udukuzi wa Kimtandao.

“Tume” maana yake ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania.

“MUVU” Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika

SURA YA KWANZA

1. UTANGULIZI

Sura hii inaelezea Chimbuko, Malengo na Walengwa ambao watahusika kutekeleza Mwongozo huu.

1.1 Chimbuko la Mwongozo

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuzingatia umuhimu wa matumizi salama, sahihi na yenye tija ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika. Chimbuko la Mwongozo huu linatokana na haja ya kuweka utaratibu unaoeleweka katika matumizi ya Mifumo ya kidijitali, vifaa vya TEHAMA, huduma za mtandao, utunzaji wa taarifa na usimamizi wa rasilimali za kielektroniki ndani ya Vyama vya Ushirika. Katika uandaaji wake, Mwongozo huu umezingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia matumizi ya TEHAMA Nchini, ikiwemo Sheria, Waraka wa Mrajis Na. 1 wa mwaka 2022 kuhusu matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Vyama Vya Ushirika, Miongozo iliyotolewa na Mrajis kuhusu matumizi ya TEHAMA, pamoja na matakwa ya Sheria ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2023. Hii inalenga kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinatumia TEHAMA kwa kuzingatia usalama wa taarifa, faragha ya Wanachama, uwajibikaji, ufanisi wa huduma na uzingatiaji wa taratibu rasmi za Serikali
kuhusu Mifumo na huduma za kidijitali.

Katika kipindi cha utekelezaji wa mageuzi mbalimbali ya kiutendaji na matumizi ya Mifumo ya kidijitali, Sekta ya Ushirika imeendelea kuonesha umuhimu wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika shughuli za Vyama vya Ushirika. Matumizi sahihi ya TEHAMA yamekuwa nyenzo muhimu katika kurahisisha usimamizi wa taarifa za Wanachama, uendeshaji wa shughuli za Vyama, utoaji wa huduma na ufuatiliaji wa maendeleo ya Sekta ya Ushirika. Hatua hizi zimechochea mafanikio ikiwemo ukuaji wa shughuli za Vyama, ongezeko la idadi ya Vyama vinavyopata hati safi na ongezeko la waajiliwa wa TEHAMA ambapo jumla ya Wataalamu wa TEHAMA.

Pamoja na mafaniko hayo, kuna changamoto mbalimbali kwenye usimamizi wa Vyama vya Ushirika ambazo ni pamoja na kuwepo kwa mianya ya ubadhirifu, kutokuwepo kwa usahihi wa daftari la Vyama vya Ushirika, takwimu za uhakika na taarifa sahihi pale zinapohitajika

na ugumu wa kupata mchango wa Vyama katika Nyanja za kiuchumi na kijamii Nchini. Kwa kiasi kikubwa changamoto hizo zinasababishwa na kiwango kidogo cha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Mifumo ya TEHAMA ina nafasi kubwa ya kuboresha na kuleta ufanisi wa uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

Katika kuimarisha uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika, Serikali kupitia Tume imeendelea kuhamasisha matumizi ya Mifumo ya nyenzo za TEHAMA ikiwepo MUVU ambao utaunganishwa na Vyama vyote vya Ushirika Nchini. Kwa kuwa utumiaji wa Mifumo unahusisha Wadau mbalimbali katika Sekta ya Ushirika ikiwemo Vyama, Tume imeandaa Mwongozo wa matumizi ya Mifumo ambao unaainisha mambo muhimu ya kuzingatia kabla na wakati wa matumizi ya Mifumo ili kuhaikisha malengo ya matumizi ya Mifumo yanafikiwa kama ilivyokusudiwa.

1.2 Malengo ya Mwongozo

Lengo kuu la Mwongozo ni kutoa utaratibu na maelekezo kwa Vyama kutambua na kufuata matumizi sahihi ya Mifumo katika uendeshaji wa shughuli za Chama ili kurahisisha uhamasishaji na usimamizi kwa mujibu wa Sheria.

Malengo mahususi ya Mwongozo ni:

a) Kujenga uelewa wa pamoja juu ya umuhimu wa matumizi ya Mifumo ya TEHAMA;
b) Kuelekeza utaratibu wa mambo ya kuzingatia kabla na wakati wa kutumia Mifumo na miundo mbinu ya TEHAMA;
c) Kuainisha vigezo na utaratibu wa matumizi ya Mifumo ya Vyama itakayounganishwa na MUVU pamoja na Mifumo mingine ya Tume na Wadau kadri itakavyo jitokeza;
d) Kuweka utaratibu wa utelekeza wa miradi ya TEHAMA katika Vyama vya Ushirika.
e) Kuelekeza mambo ya kuzingatia ili kuimarisha ulinzi wa Mifumo na taarifa;
f) Kuelekeza Vyama vya Ushirika na Wadau, kuhudumia Wanachama kwa kutumia teknolojia za kisasa na zinazo ibukia(emerging technologies) katika utekelezaji wa majukumu yake.

1.3 Walengwa wa Mwongozo

Utekelezaji wa Mwongozo huu utahusisha:

a) Vyama vya Ushirika;
b) Tume;
c) Wizara za Kisekta;
d) Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi mbalimbali za Umma zinazofanya kazi na Vyama vya Ushirika;
e) Watoa huduma; na
f) Wadau wa Ushirika

SURA YA PILI

2 HALI HALISI YA MATUMIZI YA TEHAMA

Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yanakuwa kwa kasi kubwa Duniani na hapa Nchini. Baadhi ya shughuli za uendeshaji wa Vyama, kama vile kuchapa taarifa mbalimbali, mawasiliano na kuhifadhi nyaraka na taarifa hizo zinafanywa kwa kutumia TEHAMA. Hali hii inadhihirisha kuwa TEHAMA ni sehemu muhimu ya uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika.

Kwa sasa Tume imefanikiwa kusambaza MUVU, ambao umesambazwa kutoa huduma kwa Vyama vya Ushirika na Wadau kwa njia ya Mtandao ambapo nyaraka zote zinazohitaji midhini ya Mrajis inatolewa kupitia MUVU.

Aidha, kwa upande wa Vyama vya Ushirika, vinatumia Mifumo ya TEHAMA na Nyezo za Kidigitali katika utoaji huduma kwa Wanachama na Wadau. Hadi kufikia June, 2026 jumla ya wa Vyama vya Ushirika 3,958 sawa na asilimia 60.4 ya Vyama 6,551 ambavyo vimesajiliwa kwenye MUVU tayari vimeanza kutumia Mifumo ya TEHAMA na nyenzo za TEHAMA ikiwemo Mifumo ya Kidigitali. Vilevile, vyama 196 vimefanikiwa kuajiri Wataalamu wa TEHAMA 196 ambao wana saidia vyama katika matumizi ya teknolojia ya TEHAMA.

Pamoja na hatua zilizofikiwa, bado kuna changamoto ya usimamizi na uendeshaji wa Vyama. Baadhi ya changamoto hizo ni kukosekana kwa taarifa na kumbukumbu muhimu za Chama, Mifumo duni ya mawasiliano na uhifadhi nyaraka kwenye baadhi ya vyama; uwepo wa taarifa zinazokinzana; kukosekana, uwepo wa migogoro na mashauri; ongezeko la gharama za uendeshaji pamoja na upotevu wa nyaraka na kumbukumbu za kiutendaji za Chama.

Katika kutatua changamato za uhamasishaji na usimamizi wa Vyama, Tume kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo inaendelea na jitihada mbalimbali zikiwemo kuandaa kuwezesha vyama kutumia Mifumo na nyenzo za TEHAMA katika kuendesha shughuli za Vyama.

SURA YA TATU

3 MATUMIZI YATEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Sura hii inatoa maelekezo kuhusu matumizi sahihi ya TEHAMA katika usimamizi wa Vyama vya Ushirika na kufafanua mambo ya kuzingatia kabla na wakati wa utumiaji.

3.1. Mambo ya kuzingatia kabla ya kutumia Mifumo na nyenzo za TEHAMA.

3.1.1. Vitendea kazi

Chama kitatakiwa kununua vitendea kazi vya TEHAMA kulingana na ukubwa wa Chama, eneo kilipo, mahitaji ya matumizi katika kuendesha shughuli za Chama. Chama kinaweza kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa Mtaalamu wa TEHAMA.

3.1.1.1. Kompyuta

Chama kinatakiwa kuwa na kompyuta mpakato au Kompyuta ya mezani ambayo itawezesha kutumia mtandao kwa ajili ya kufikia Mfumo. Kiwango cha chini cha vigezo msawazo kwa vifaa hivi kimeambatishwa kama ***Kiambatisho Na.1.*** na ***Kiambatisho Na.2*****.**

3.1.1.2. Printer/Scanner au Photocopier

Kwa ajili ya kurahisisha uchapishaji na upatikanaji wa nakala ngumu chama kinatakiwa kuwa na vifaa hivi kutoka kwenye Mfumo. Kiwango cha chini cha vigezo msawazo kwa vifaa hivi kimeambatishwa kama ***Kiambatisho Na.3.***

3.1.1.3. Kishkwambi

a) Chama cha Ushirika kinaweza vishkwambi kama sehemu ya vitendea kazi vya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha ukusanyaji, uingizaji, uhakiki na uwasilishaji wa taarifa za chama kwa njia ya kidigitali.

b) Chama kihakikishe Kifaa hiki na sifa na viwango elekezi kwa ajili ya kuweza kutunza programu mbalimbali na kufanya kazi maeneo ambayo hayana mtandao na yenye mtandao. Kiwango cha chini cha vigezo msawazo kwa vifaa hivi kimeambatishwa kama ***Kiambatisho Na.6.***

3.1.1.4. Point of Sales Device (POS)

a) Chama kinaweza kuwa na **POS yenye mtandao** ambayo itakisaidia Chama katika kukusanya taarifa hasa maeneo yenye changamoto ya mtandao au Mtendaji wa Chama atakapokuwa anakusanya taarifa nje ya Ofisi.

b) Kifaa hiki lazima kiwekewe programu (App) inayoweza kutunza taarifa eneo ambalo halina mtandao wa Internet na baada kuzituma kwenye Mfumo moja kwa moja pindi kinapofikishwa sehemu yenye Mtandao. Kiwango cha chini cha vigezo msawazo kwa vifaa hivi kimeambatishwa kama ***Kiambatisho Na.4.***

3.1.1.5. Kifaa cha kupata Mtandao

a) Chama kinatakiwa kuwa na kifaa ambacho kitasaidia kupata mtandao kulingana na eneo la kijiografia ambapo Chama kinaendesha shughuli zake.

b) Aina ya vifaa hivyo ni: **"Modem" & Rauta",** "**Simu Janja"** na **Fiber,** Mkonga wa Taifa, mawasiliano ya Makampuni ya Simu**.** Hivyo**,** kupitia mojawapo ya vifaa hivi kila Chama kitatakiwa kununua kifurushi cha data kulingana na mahitaji yake ili kupata huduma ya mtandao.

3.1.1.6. Mizani ya Kidigitali

a) Chama cha Ushirika kinachojihusisha na shughuli za uzalishaji, ukusanyaji, ununuzi, au mauzo ya mazao na bidhaa kinatakiwa kuwa na Mizani ya Kidigitali kwa ajili ya kupima uzito kwa usahihi na kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za makusanyo ya Mwanachama kwenye Mfumo.

b) Chama kinatakiwa kuhakikisha kuwa Mizani ya kidijitali isiwe na program iliyofungwa na Mtoa huduma na kuzuia kutumika kwa mahitaji ya Chama na Wadau wake (Vender locked)

c) Chama kihakishe Mizani ya Kidigitali inaunganishwa na Mfumo wa Chama moja kwa moja uwezo wa kuunganisha na Watoa huduma mbalimbali

d) Chama kihakikishe Mtoa huduma anawasilisha nyaraka za kiufundi za namna yakuunganisha Mizani na kuifanyia ukarabati Kinga na uhuishaji

e) Kiwango cha chini cha vigezo msawazo kwa vifaa hivi kimeambatishwa kama ***Kiambatisho Na.5.***

f) Mfumo wa Mizani uruhusu mawasiliano au kuunganishwa moja kwa moja kama ilivyoainishwa kwenye Mchoro Na. 1 hapo chini.



Mchoro Namba 1: Mfumo wa Mizani za Kidigitali

3.1.1.7. Mashine ya Kutolea Huduma za Kifedha (ATM)

Chama au Taasisi ya Ushirika inayotoa huduma za kifedha kwa Wanachama wake inaweza kuwa na Mashine ya Kutolea Huduma za Kifedha (ATM) kwa ajili ya kuwezesha Wanachama kupata huduma mbalimbali za kifedha kwa urahisi na wakati wowote. Huduma hizo zinaweza kujumuisha kutoa fedha, kuangalia salio la akaunti, kufanya miamala mbalimbali na kupata taarifa za kifedha.

Kwa kuwa matumizi ya ATM yanategemea aina na ukubwa wa shughuli za Chama husika, sifa za kifaa hicho zitaamuliwa kwa kuzingatia mahitaji ya Chama na ushauri kutoka , Taasis za fedha husika.

3.1.1.8. Chumba cha Seva

Katika mazingira ya kisasa ya kidijitali, Vyama vya Ushirika vinahifadhi na kutumia taarifa nyingi muhimu kama taarifa za Wanachama, miamala ya kifedha, taarifa za mikopo, kumbukumbu za biashara, na Mifumo ya uendeshaji. Ili kulinda taarifa hizi dhidi ya upotevu, wizi wa taarifa, au

matumizi ya taarifa ambayo hayajaidhinishwa, ni lazima Chama kutenga chumba maalum cha Seva chenye viwango vya ulinzi na usalama unaofaa ikiwemo uwepo wa *CCTV* kamera, mlango unaofungwa na kufunguliwa na Mtu maalum ambae atawajibika.

3.1.2. Ununuzi wa Vitendea Kazi

Kila Chama kitatakiwa kutenga kasma ya ununuzi na matengenezo ya vitendea kazi tajwa sehemu ya 3.1.1 katika mpango wa makisio ya mapato na matumizi. Aidha ununuzi wa vifaa hivi utekelezwe kwa kuzingatia Mwongozo wa manunuzina ugavi.

3.1.3. Mabadiriko ya Teknolojia ya Vifaa na Nyenzo za TEHAMA

Kutokana na TEHAMA kukua kwa kasi na kuwepo kwa mabadiriko ya mara kwa mara Chama kinaruhusiwa kununua vifaa hivi vyenye sifa za juu zaidi baada ya kuomba ushauri kutoka kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

3.1.4. Mafunzo

Chama kihakikishe kupitia tengo la elimu na mafunzo kinawajengea uwezo wa masuala ya TEHAMA Viongozi na Watendaji.

3.1.5. Anwani ya Barua Pepe

Kila Chama kinatakiwa kuwa na barua pepe pamoja na namba ya simu kwa ajili ya mawasiliano kuwezesha kuunganishwa kwenye Mfumo. Barua pepe ya Chama ianze na jina la Chama, kwa mfano: **jina la chama@gmail.com**. Hata hivyo, Chama chenye Kikoa **(*Domain*)** kinatakiwa kutumia kikoa chake katika kutengeneza email.

3.2. Kuwasilisha taarifa kupitia Mfumo Mama wa Tume wa MUVU.

i. Kila chama kinatakiwa kuhakikisha taarifa zote za Usimamizi na uendeshaji zinaingizwa kwenye MUVU.
ii. Chama kitatakiwa kuhakikisha kinaunganisha Mfumo wake na MUVU na taarifa zinatumwa kwenye MUVU kutokea Mfumo wa Chama.

3.3. Msaada wa Kiufundi

Chama kihakikishe kinapata msaada wa kitaalamu juu ya Mfumo au nyenzo za TEHAMA, kiwasiliane na Tume kupitia barua pepe ya ,ict@ushirika.go.tz au piga namba ya huduma kwa wateja bila malipo **0800110105 au 0800110104**.

SURA YA NNE

4 MIFUMO YA TEHAMA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Sura hii inaeleza matumizi ya TEHAMA kwenye Vyama, hususani utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa na Vyama wakati wa ununuzi wa Mifumo au nyenzo za TEHAMA na uendeshaji wake.

4.1. Mfumo wa Uendeshaji wa shughuli za Chama

i. Chama kihakikishe kinazingatia nyaraka na Miongozo iliyotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika inayopatika Katika Tovuti ya Tume Kupitia anuani ya www.ushirika.go.tz/

   a. Mwongozo wa Sifa na Viwango(Softaware requirement Specification- SRS) vya Mfumo kwa Vyama visivyo Vya Kifeza

   b. Mwongozo wa Sifa na Viwango (SRS) kwa Vyama vya Kifedha;

   c. Sera ya kudhibiti matumizi ya Taarifa (Data access Policy)

   d. Sera ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwenye Vyama Vya Ushirika (Data Privacy and Protection Policy)

   e. Sera ya Usalama Mtandao (Cyber Security Policy)

   f. Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binfasi ya Mwaka 2023 kutoka Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)

ii. Kwa Vyama vya Msingi ambavyo uwezo wake na shughuli zake ni ndogo. Chama Kikuu kihakikishe kinazingatia kuweka Moduli na Dirisha la Vyama Wanachama hao ili kuwezesha utunzaji wa Taarifa na kupunguza gharama. Aidha, Moduli hiyo iwe na uwezo wa angalu kuwezesha Chama cha Msingi kufunga Hesabu, kuandaa Bajeti, taarifa za Chama na Wanachama na taarifa Masoko na hisa kulingana na aina ya Chama.

iii. Chama kihakikishe kuwa kinatengeneza Mfumo mwepesi ***(Light weigth Version)*** unaoweza kufanya kazi kwenye Mtandao ***(online)*** na pale pasipo na Mtandao ***(offline)*** na Mfumo huo

uweze kuwasiliana na Mfumo mama kwenye eneo lenye mtandao na ifanye moja kwa moja ***(auto Synchronization).***

iv. Kwa mazingira yenye changamoto ya nishati ya Umeme Chama kijikite kwenye matumizi ya nishati mbadala ya jua ***(solar power).***

v. Vyama vinashauri kuwekeza kwenye Teknolojia ya kisasa kama Internet of Things (IoT), akili unde na Chatbot ili kuwezesha matumizi ya kidijitali kuchochea mabadiliko ya haraka na kuleta matokeo kwa Vyama, Wanachama na Taifa kwa ujumla.

vi. Chama kihakikishe kuwa Mizani ya kidigitali au kifaa chochote cha nyenzo ya TEHAMA ni mali ya Chama na haijafungwa ***(Not vendor locked)*** na Muuzaji ili kurahisisha kuunganisha na Mfumo wa Chama bila kumtegemea Muuzaji au Mzabuni;

vii. Chama Kihakikishe kuwa kinaandaa vigezo na Sifa vya Mfumo ambao Chama kinataka kununua/Kutengeneza vimewasilishwa kwa Tume kwa ajili kupata ushauri wa kitaalamu kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi au nyenzo za TEHAMA.

viii. Kuhakikisha kuwa Mfumo unatengenezwa na uwezo wa kuunganishwa kwa usalama ***(secure and effiecient)*** na MUVU au Mifumo mingine ya Tume na Wadau kadri itakavyokuwa inaongezeka;

ix. Usanifu wa Mifumo uzingatie matumizi ya programu na Teknolojia za TEHAMA za sasa na zijazo ***(emerging Technology);***

x. Mfumo uwe na uwezo wa kutumia na kupokea kutoka Mifumo mingine kama MUVU kwa kutumia Teknolojia ya REST API;

xi. Kuhakikisha ulinzi na Usalama wa Taarifa kutokana na upotevu, kutolewa bila kibali, uharibifu, kuibwa, kubadirishwa kwa nia ya kupotoshwa, ***(alteration),*** uvamizi wa kimtandao na kutumika pasipo ruhusa;

xii. Kuhakikisha kila Mtumiaji wa Mfumo anapewa haki ya kutumia Mfumo kulingana na Majukumu yake; Rejea ”Data Access Policy” iliyo kwenye Tovuti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

xiii. Kwa ajili ya kupunguza udukuzi Chama kihakikishe Mfumo wenye Taarifa muhimu unatumia Teknolojia ya Uthibitisho wa aina Mbili ***(Two-Factor Authentication 2FA)*** wakati

wa kufungua akaunti kwenye Mifumo. (Mfano. nenosiri + msimbo maalum unaotumwa kwenye Simu yako).

ix . wajibu wa kila Mtendaji wa Chama kuhakikisha kwamba anahifadhi kikamilifu nywila yake ya kuingia kwenye Mfumo na Mtu mwingine hawezi kuifahamu au kuinakili kwa namna yoyote ile; na



Mchoro Namba 1: Uthibitisho wa Aina mbili (2FA)

x. Kuhalkikisha taarifa za Chama haziuzwi, kuchakatwa, kutangazwa kibiashara, kuzigawa, kuzisambaza kwa njia yoyote kwa mtu mwingine ***(Third Party)*** pasipo idhini ya Uongozi wa Chama cha Ushirika au Msimamizi (***Mrajis wa Vyama vya Ushirika***)

xi. Chama kikuu kuweke utaratibu na kuhakikisha kuwa kuna Mbadala wa utunzaji wa Taarifa (Backup Server) nje ya chumba au jengo kilichotengwa ili kujiepusha na majanga ya upoteaji wa Taarifa iwapo yatatokea;

xii. Chama kuhakikisha kinakuwa na hati miliki ya Mfumo na kutenga Bajeti ya kuhuisha Mfumo kadri mahitaji yapotokea.

xiii. Chama kuhakikisha kwamba endapo mkataba kati yake na mmiliki wa Mfumo utakoma au kusitishwa kwa namna yoyote ile kinabaki na taarifa na kumbukumbu zake kabla ya kusitishwa huduma ya Mfumo husika.

4.2. Usalama wa Programu na Vifaa vya TEHAMA

(i) Chama kihakikishe kuwa kompyuta zote zinawekewa programu ya kukinga na kuondoa virusi na kihakikishe kuwa programu hizo zinahuishwa mara kwa mara;

(ii) Chama kinapaswa kulinda usalama wa kompyuta kwa kuepuka kupakua programu hatarishi kutoka kwenye mtandao;

(iii) Chama kinapaswa kuhuisha Sera za udhibiti wa ndani ili zijumuishe mahitaji ya ulinzi na usalama wa matumizi na vifaa vya TEHAMA;

(iv) Kiongozi na Mtendaji wa Chama anayetaka kutumia vitunza au vihamisha kumbukumbu kutoka kwenye kompyuta anapaswa kufanya “virus scanning” kabla ya kutumia vifaa hivyo; na

(v) Inapojitokeza hitilafu ya kiufundi kwenye vifaa vya TEHAMA na kulazimika kuleta Mtaalamu kutoka nje ya Ofisi, Mtaalamu huyo atasimamiwa na Mtendaji wa Chama kwa muda wote anapofanya kazi.

SURA YA TANO

5 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Sura hii inaelezea wajibu wa Bodi ya Uongozi wa Chama, Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Mkaguzi wa Nje, Watoa huduma, Mfilisi wa Chama na Wadau wa maendeleo ya Ushirika, muda wa kuanza kutumika na mapitio ya Mwongozo huu.

5.1. Wajibu wa Chama

a) Kukusanya, kuhifadhi na kuhuisha taarifa kwenye Mfumo;
b) Kuhakikisha kuwa taarifa zote zilizohifadhiwa kwenye Mfumo zinakuwa siri isipokuwa taarifa zisizomtambulisha Mwanachama kwa Wadau wengine baada ya taarifa hizo kujadiliwa na kuidhinishwa na Bodi ya Chama;
c) Kumuwezesha kila Mwanachama kupata taarifa zake kwa wakati na kwa urahisi mara anapozihitaji;
d) Kuoanisha Mfumo na Mifumo mingine ya utendaji kazi iliyopo chamani;
e) Kutunza na kulinda vifaa vya TEHAMA;
f) Kutoa taarifa kwa Afisa Ushirika juu ya mabadiliko ya Watendaji wa Chama waliosajiliwa kwenye Mfumo;
g) Kuwasiliana na Tume panapokuwa na changamoto za utekelezaji wa Mwongozo; na
h) Kupitia, kuuelewa na kuhakikisha Mwongozo unatekelezwa kikamilifu.

5.2. Wajibu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika

a) Kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo huu;
b) Kutathmini utekelezaji wa matumizi ya Mfumo; na
c) Kupitia na kuhuisha Mfumo ili uendane na mabadiliko kadiri itakavyohitajika.
d) Kuhuisha taarifa za Chama
e) Kuhakikisha Mifumo yote inayoombewa vibali na Watoa huduma inakizi vigezo vya kuunganishwa na MUVU na Mifumo mingine ya Tume kadri itakavyoongezeka.

5.3. Wajibu wa Mkaguzi wa Nje

Kuhakikisha kuwa Chama kimezingatia matakwa ya Mwongozo huu.

5.4. Wajibu wa Watoa Huduma

(i) Kuomba kibali kutoka Tume kupitia MUVU ili kutoa huduma ya TEHAMA kwenye Vyama; na

(ii) Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wakati wa kutoa huduma ya TEHAMA kwenye Vyama.

5.5. Wajibu wa Mfilisi

Kuwasilisha taarifa za ufilisi kupitia MUVU

5.6. Wajibu wa Wadau wa Maendeleo ya Ushirika

Kushirikiana na Vyama na Tume katika uendelezaji wa Mifumo ya TEHAMA katika Vyama.

5.7. Muda wa kuanza kutumika

Mwongozo huu utaanza kutumika mara utakapotiwa saini na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

5.8. Mapitio

Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu (3) au itakapotokea mabadiriko ya sera,sheria,,kanuni au Teknolojia

6 VIAMBATISHO

6.1. **Kiambatisho Na.1:** Mapendekezo ya Sifa za Kompyuta Mpakato

Features	Minimum Specifications
Operating System	**Genuine** Microsoft Windows 10 (32 Bit)
Processor	Intel Core i5-13420H, 8 cores, up to 4.6 GHz turbo frequency, part of the 13th Gen Intel Core family
Memory	RAM 8 GB or above
Hard Disk Drives	512 GB or above
Audio	Bang & Olufsen, dual speakers, Audio Boost with all installed drivers
Communications/Wireless Support	Integrated Network Card (LAN): 10/100/1000mbps WLAN: 802.11 ac Wireless LAN or latest USB 3.0 Connectivity, 2 Slots or More Mobile Broadband Module (Recommended)
I/O Devices	Keyboard: Illuminated Backlit, Spill-resistant keyboard with drain Webcam: Yes
Supplemental Items	Stereo headphone / Microphone Combo CD/DVD, R/RW Drive: Internal or External Leather Case Mouse Graphics: NVIDIA RTX (128 MB or Better Business Class)
Display	14” (35.5 cm) diagonal FHD IPS BrightView micro-edge WLED-backlit (1920 x 1080)
Software	Genuine Microsoft Office 2021 or above
Minimum Warrant	12 Months

Kiambatisho Na.2: Mapendekezo ya Sifa za Kompyuta ya Mezani

Features	Minimum Specifications
Operating System	**Genuine** Microsoft Windows 11 (64 Bit)
Processor	Intel ® Core i5 or above
Memory	RAM 8 GB or above
Hard Disk Drives	512 GB or above
Video Card	Intel ® Integrated Graphics
Ports	At least 5 USB 2.0 or 3.0 Standard Serial Port, 1 Parallel Port 1 VGA Port, Audio In/Out

Keyboard	USB Standard Keyboard
Ponting Device	USB Optical Scroll Mouse
Display	HDMI or DVI Support
Monitor	24 Monitor or above
Connectivity	Integrated Gigabit Ethernet, 802.11b/g/n Wireless Interface
Others	Build in Speakers
DC/DVD, R/RW Combo	Internal
Software	Genuine Microsoft Office 2021 or above
Minimum Warrant	12 Months

6.2. Kiambatisho Na.3: Mapendekezo ya Sifa za Printa

Features	Minimum Specifications
Model	Pro MFP M428dw
Display	6.8 cm (2.7 in)
Printing Speed	Up to 45ppm
Copying Speed	Up to 38 cpm
Duplex Printing Mode	Auto
Duplex Function	Copy, Print, Scan
Print Technology	Laser Black
Memory	80MB or higher, Expendable
Media Sizes, Custom	Tray 1: 76.2 x 127 to 215.9 x 355.6 mm; Tray 2, 3: 104.9 x 148.59 to 215.9 x 355.6 mm
Connectivity	1 rear host USB and 1 Front USB port
	Gigabit Ethernet 10/100/1000BASE-T network; 802.3az (IEEE - 1284); 802.11b/g/n/2.4/5 GHZ
	Integrated Bluetooth 4.2
Minimum Warrant	12 Months

6.3. Kiambatisho Na.4: Mapendekezo ya Sifa za POS TPS 390

Features	Minimum Specifications
Operating System	**Android 12.0** or above
Processor	Quad-Core 1.1GHz or above
Memory	4GB DDR, 16GB eMMC
Display	5-inch, 720*1280
Keypads	12 Alphanumeric Keys, 2 Function Keys

Thermal Printer	Paper width: 58mm, 35mm
Magnetic Card Reader	Track 1/2/3, bi-directional swipe, ISO 7810, ISO 7811, ISO 7812
Smart Card Reader	ISO 7816
SIM Slots	2 SIM
SAM Slots	2 SAMs
Contactless Card Reader	ISO 14443 Type A/B, Mi Fare
Camera	5M Pixel, Auto Focus (Barcode Software Decoding)
Peripheral Ports	1 Micro USB(OTG), 1 Mini USB, 1 DC Charge
	1 Audio Jack
Power Supply	5V/2A
MDM	Mobile Device Management
Battery	7.4V/2500mAh, Li-ion
Certification	CE, FCC
GPS	Built-in
Minimum Warrant	12 Months

6.4. Kiambatisho Na. 5: Mapendekezo ya Sifa za Mizani ya Kidigitali

Features	**Minimum Specifications**
Type	Digital Platform Scale / Electronic Weighing Scale
Weighing Capacity	300Kg or above, kulingana na aina ya mazao au bidhaa zinazopimwa na Chama
Accuracy / Precision	50g – 100g or better
Measurement Unit	Kilogram (Kg)
Display	Digital LCD/LED display yenye mwanga na inayosomeka kwa urahisi
Customer Display	Display ya ziada kwa ajili ya mwanachama/mteja kuona uzito uliopimwa
Platform Size	600mm x 800mm or above kwa ajili ya kupima magunia, mazao au bidhaa kubwa
Platform Material	Heavy duty steel / stainless steel, isiyoshika kutu kwa urahisi
Power Supply	AC 220V–240V, 50Hz

Battery Backup	Rechargeable battery inayoweza kufanya kazi angalau saa 6–8 bila umeme
Tare Function	Iwe na uwezo wa kutoa uzito wa kifungashio/kontena kabla ya kupima bidhaa
Zero Function	Iwe na uwezo wa kurudisha kipimo katika sifuri kabla ya matumizi
Connectivity	USB, RS232 au Bluetooth kwa ajili ya kuunganisha na POS, kompyuta au Mfumo wa Chama
Data Export	Iwe na uwezo wa kusafirisha taarifa za vipimo kwenda kwenye mfumo au kifaa kingine pale inapohitajika
Printing Support	Iweze kuunganishwa na printer ya risiti au label printer kwa ajili ya kuchapisha taarifa za vipimo
Calibration	Iwe na uwezo wa kufanyiwa calibration na uthibitisho wa vipimo kwa mujibu wa taratibu za mamlaka husika
Environmental Protection	Iwe na kinga dhidi ya vumbi na unyevunyevu, angalau IP54 or above
Operating Temperature	0°C to 40°C or above
Security	Iwe na mfumo wa kulinda settings muhimu ili kuzuia mabadiliko yasiyoidhinishwa
Accessories	Charger, rechargeable battery, user manual, data cable na calibration certificate
Warranty	Minimum warranty ya miezi 12
After Sales Support	Mtoa huduma awe na uwezo wa kutoa matengenezo, vipuri na msaada wa kiufundi ndani ya nchi
Software Program	Mizani isiwe na program iliyofungwa na Mtoa huduma mmoja pekee Iwen a uwezo wa kuunganisha na watoa huduma mbalimbali Mtoa huduma atoe nyaraka za kiufundi za namna yakuunganisha Mizani na Mifumo mingine

Mizani ya kidigitali itakayonunuliwa na Chama inapaswa kuwa imara, sahihi, rahisi kutumia na yenye uwezo wa kuunganishwa na vifaa vingine vya TEHAMA kama vile POS, kompyuta au Mfumo wa uendeshaji wa Chama ikiwa sambamba na kuunganishwa na
Mfumo wa MUVU.

6.5. Kiambatisho Na.6: Mapendekezo ya sifa za vishikwambi

FEATURES	MINIMUM SPECIFICATIONS
Device Type	Tablet / Kompyuta Kibao / Kishkwambi
Operating System	Android 16 or above / iPadOS equivalent / Windows Tablet OS equivalent
Processor	Octa-Core Processor, 2.0GHz or above
Memory RAM	8GB RAM or above
Internal Storage	128GB or above, expandable storage recommended
Display Size	8 inches or above
Display Resolution	HD display, 1280 x 800 pixels or above
Touch Screen	Capacitive multi-touch screen
Connectivity	Wi-Fi 802.11 a/b/g/n/ac or latest
Mobile Network Support	4G LTE or above, SIM Card support recommended
Bluetooth	Bluetooth 5.2.3 or above
GPS	Built-in GPS for location-based field activities
Camera	Rear Camera 8MP or above; Front Camera 5MP or above
Ports	USB Type-C charging/data port; OTG support recommended
Battery Capacity	5,000mAh or above
Battery Life	Minimum 6–8 hours of normal usage
Audio	Built-in speaker and microphone
Security Features	Password, PIN, pattern, fingerprint or face unlock support
Data Security	Device encryption and remote lock/wipe capability recommended
Application Support	Compatible with web browser, PDF reader, office document viewer, data collection applications and cooperative management systems
Device Management	Mobile Device Management (MDM) support recommended
Durability	Protective cover/casing and screen protector recommended

Accessories	Charger, USB cable, protective cover, screen protector and user manual
Warranty	Minimum warranty of 12 months
After Sales Support	Suppliers must provide technical support, maintenance and spare parts availability within the country

6.6. Kiambatisho Na.7: Mapendekezo ya sifa za Simu janja za Mkononi

Feature	**Minimum Specifications**
Operating System	Android 12 (can be updated up to current Android
Display	6.8-inch Dynamic AMOLED 2X, QHD+ (1440 × 3088), 1–120Hz Adaptive Refresh Rate
Processor	Qualcomm Snapdragon 8 Gen 1 (OR Exynos 2200 in some of the market)
RAM	8GB/12GB
Storage	128/256GB
MicroSD	No MicroSD slot
Real Camera	108MP (Main) + 12MP (Ultra-Wide) + 10MP (3x Telephoto) + 10MP (10x Periscope Telephoto)
Front Camera	40MP
Zoom	3x Optical Zoom, 10x Optical Zoom, hadi 100x Space Zoom
Battery	5,000mAh
Charging	45W Wired Fast Charging, 15W Wireless Charging, Wireless PowerShare
S Pen	Built in
Water Resistance	IP68 Dust & Water Resistant
Connectivity	5G, Wi-Fi 6E, Bluetooth 5.2, NFC, USB Type-C
Fingerprint	Ultrasonic In-Display Fingerprint Sensor
Dimensions	163.3 × 77.9 × 8.9 mm
Weight	229g

